TN Department of Education

# Kujiunga na Darasa la Tatu: Mwongozo wa Rufaa ya Mzazi

Katika mwaka wa 2021, Bunge Kuu la Tennessee lilirekebisha T.C.A. § 49-6-3115, sheria ya jimbo kujiunga na darasa linalofuata kutoka darasa la 3 ambayo inahakikisha kuwa wanafunzi wanaohitaji usaidizi wa ziada wanaweza kuupokea kabla ya kujiunga na darasa la 4. Bodi ya Elimu ya Jimbo (SBE) ilitangaza sheria za kuanzisha mchakato wa kukata rufaa kwa wanafunzi ambao wametambuliwa kuwa watarudia darasa la tatu.

**Je, ni nani anaweza kukata rufaa?**

- Mzazi au mlezi anaweza kukata rufaa kwa niaba ya mwanafunzi wake.
- Mzazi au mlezi wa mwanafunzi pia anaweza kutia saini kwenye fomu ya kutoa idhini kwa mwakilishi wa shule ya wilaya au shule ya umma inayojitegemea kujaza fomu ya rufaa ya mwanafunzi wao kwa niaba yao. Unaweza kupata fomu hiyo ya Idhini ya Rufaa kwenye ukurasa wa tovuti ya Uboreshaji wa Mafunzo .

**Je, ninaweza kukata rufaa wakati gani?**

- Kipindi cha rufaa hufunguliwa kuanzia Mei 28 – Juni 27, 2025. Rufaa zote sharti ziwasilishwe wakati wa kipindi cha rufaa ili kuzingatiwa.

**Je, ni nani anastahiki kukata rufaa?**

- Wanafunzi waliopata alama “inayokaribia kutimiza matarajio” kwenye mjarabu wao wa ELA TCAP au ELA TCAP waliofanya tena.
    - Je, ikiwa mwanafunzi wangu alipata alama “inayotimiza matarajio” au “inayozidi matarajio” kwenye mjarabu wake wa ELA TCAP au ELA TCAP aliyorudia?
        - Hayuko kwenye hatari ya kurudia, kwa hivyo ukataji rufaa hauhitajiki.
    - Je, ikiwa mwanafunzi wangu alipata alama ya “chini ya kiwango cha matarajio?”
        - Wanafunzi pekee waliopata alama “inayokaribia kutimiza matarajio” ndio wanaostahiki kukata rufaa kulingana na sheria. Tembelea ukurasa wa tovuti ya Uboreshaji wa Mafunzo kwa ajili ya kufahamu njia zinazopatikana za kujiunga na darasa la nne na uwasiliane na mwalimu mkuu wa mwanafunzi wako.

**Je, masharti ya uidhinishaji wa rufaa ni yapi?**

Wazazi au wawakilishi wa wilaya walioteuliwa wanaweza kukata rufaa kwa kuzingatia mojawapo ya sababu hizi mbili:

**Misingi ya Sababu ya 1:**
Rufaa kwa misingi ya sababu ya 1 ina vigezo vinne ambavyo sharti vizingatiwe.

1. Mwanafunzi amepata alama sawa au zaidi ya asilimia arobaini (40%) kwenye mjarabu uliotolewa majira ya kuchipua wa TN-URS (Aimsweb).
2. Mwalimu mkuu wa shule anakubali kuunda mpango wa kurekebisha masomo kwa ajili ya mwanafunzi huyo.
3. Mwalimu wa somo la ELA na mwalimu mkuu wa mwanafunzi hutoa pendekezo kwa kauli moja la kujiunga na darasa linalofuata.
4. Shule ya wilaya au shule ya umma inayojitegemea ya mwanafunzi inakubali kutoa huduma za mafunzo ya viwango vya juu vya uwiano wa chini kwa mwaka mzima wa shule wa darasa la nne kwa mwanafunzi.

**Misingi ya Sababu ya 2:**
Rufaa kwa misingi ya sababu ya 2 inaeleza kuwa msiba ulitokea katika au ndani ya siku 60 za kalenda kabla ya tathmini ya TCAP ambao uliathiri uwezo wa mwanafunzi wa kuonyesha ujuzi wa sasa kwenye mjarabu.

Mifano ya tukio la msiba ni pamoja na, lakini sio tu:

- Kifo katika familia yake
- Upotezaji wa makazi
- Utambuzi wa kimatibabu wa ugonjwa hatari

**Je, ni maelezo gani ninayohitaji ili kuwasilisha rufaa?**

- **Maelezo ya Mwanafunzi:** Jina la kisheria na tarehe ya kuzaliwa
- **Maelezo ya Mzazi au Mwakilishi aliyeteuliwa wa Wilaya ya Shule au Shule ya Umma Inayojitegemea:** Jina, barua pepe na nambari ya simu
- **Kitambulisho cha Jimbo cha Mwanafunzi:** Nambari yenye tarakimu 7 inayoweza kuombwa kutoka kwa shule ya mwanafunzi wako. SSID isiyo sahihi inaweza kuchelewesha kasi ya ukaguzi.
- **Misingi ya Sababu ya 1:** Fomu iliyojazwa ya Pendekezo la Rufaa kwa Misingi ya sababu ya 1 (inayopatikana kwenye ukurasa wa tovuti waUboreshaji wa Mafunzo ) ikiwa imewekwa sahihi zote zinazohitajika kutoka kwa mwalimu mkuu wa mwanafunzi wako na mwalimu wa somo la ELA. Utahitajika kupakia nakala ya fomu hiyo unapowasilisha ombi la rufaa.
- **Misingi ya Sababu ya 2:** Maelezo ya msiba yayoumuisha tarehe na maelezo yanayoeleza jinsi tukio kutokea kwenye au ndani ya siku 60 za kalenda kabla ya tathmini ya TCAP lilivyoathiri uwezo wa mwanafunzi wa kudhihirisha ujuzi wa sasa kwenye mjarabu.

**Je, rufaa hufanya kazi vipi?**

Wazazi au wawakilishi walioteuliwa wa wilaya ya shule au shule ya umma inayojitegemea watajaza Fomu ya Kukata Rufaa dhidi ya Uamuzi wa Kurudia Darasa la tatu kwenye ukurasa wa tovuti wa Uboreshaji wa Mafunzo na kukata rufaa kwa misingi ya mojawapo ya sababu hizi mbili. Rufaa hiyo itatathminiwa na idara na uamuzi utatolewa ndani ya siku 14 kufuatia uwasilishaji mradi tu maelezo yote ni kamili na sahihi.